**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NAMAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET)**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MATOKEO YA UHAKIKI WA WANAFUNZI MKUPUO WA MACHI 2026**

Baraza linautaarifu umma kuwa matokeo ya uhakiki wa waombaji waliochaguliwa kujiunga na masomo Muhula wa Machi, 2026 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada yametangazwa rasmi leo tarehe **31 Machi, 2026.**

Jumla ya waombaji 8,911 kati yao wanawake 5,028 (56.4%) na Wanaume 3,883 (43.6%) waliwasilishwa kwa ajili ya uhakiki kutoka katika vyuo vilivyokidhi vigezo vya kudahili katika mkupuo wa Machi 2026. Kati ya waombaji hao 8,713 (97.8%), wanawake 4,935 na wanaume 3,778 walikuwa na sifa za kujiunga na programu walizoomba. Aidha, waombaji 198 (2.2%) hawakuwa na sifa katika programu walizoomba.

Waombaji wote walioomba kujiunga katika programu mbalimbali wanaweza kupata taarifa zao za uhakiki kwa kutumia msimbo uliotumwa kwenye namba ya simu kwa kubonyeza kitufe cha“***Angalia Hali ya Uhakiki wa Muhula wa Machi 2026”*** au “***Uhakiki mkupuo wa Machi, 2026”*** katika tovuti ya Baraza **www.nactvet.go.tz**. Baraza linasisitiza kila mwombaji mwenye sifa ya kudahiliwa kutunza msimbo aliotumiwa kwani ndio utatumika katika udahili mara wafikapo chuoni.

Baraza linavielekeza vyuo kuwasajili wanafunzi wenye sifa na watakaowasili vyuoni kwa ajili ya kuanza masomo tarehe **27 Aprili, 2026,** kwa kutumia misimbo iliyotumwa na Baraza kwenye namba za waombaji. Hatua Stahiki zitachukuliwa kwa Chuo kitakachokiuka taratibu za udahili.

Aidha, vyuo vimepewa nafasi ya kurekebisha na kuwasilisha taarifa za waombaji ambazo hazikuwa sahihi kuanzia tarehe **20 - 26 Aprili, 2026.**

**IMETOLEWA NA:**
**KATIBU MTENDAJI**
**(NACTVET)**
**31 MACHI, 2026**